# TAARIFA YA MKUU WA MKOA WA MTWARA
# JUU YA MASUALA MBALIMBALI YANAYOHUSU
# BIASHARA YA KOROSHO KATIKA
# MKOA WA MTWARA

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Kwanza kabisa napenda kutumia nafasi hii kuwakaribisha katika kikao hiki kifupi kinachoelezea au kutoa ufafanuzi wa mambo mbalimbali yahusuyo ukusanyaji, usafirishaji na bei ya korosho katika msimu huu wa mwaka 2017/2018.

Awali ya yote niseme kuwa mimi ni mgeni katika Mkoa hata hivyo ugeni wangu sio kigezo cha kushindwa kutoa maelekezo au maagizo ya serikali katika kipindi hiki cha msimu ambapo serikali imekusudia kuhakikisha kuwa mkulima anapata bei nzuri ya korosho na analipwa kwa wakati. Aidha, serikali ina kusudia kuzuia na kupambana na biashara haramu ya Kangomba au Chomachoma. Kwa upande mwingine serikali inataka kuona Bandari ya Mtwara kuwa njia pekee ya kusafirisha korosho zilizozalishwa katika mikoa hii ya kusini. Katika kutimiza hayo yote serikali ya mkoa wa Mtwara inaheshimu haki zote za wadau wa Korosho ikitanguliza mbele maslahi ya taifa na kukuza uchumi wa Wanamtwara.

**Ndugu waandishi wa Habari,**

Kutokana na utangulizi huo nilioutoa hapo mwanzo naomba sasa nitoe ufafanuzi wa baadhi ya mambo na msimamo wa baadhi ya masuala juu ya mwenendo wa biashara ya korosho kwa msimu huu kama ifuatavyo: -

**(a) <u>Bei ya korosho</u>**

Kwanza ununuzi wa korosho kwa kutumia mfumo wa Stakabadhi Ghalani umeshaanza mapema mwezi wa Oktoba, 2017, Minada minne/mitatu imeishafanyika na Tani 48,172.6 za korosho zimeshanunuliwa na jana (tarehe 3/11/2017) minada miwili imefanyika Tandahimba (TANECU) na Nanyumbu (MAMCU). Bei ilikuwa kati ya Tshs. 3,970 na 4007. Kuna mwitikio mkubwa wa wafanyabiashara wanaotaka kununua korosho na hivyo kutoa mwelekeo kuwa bei itaendelea kupanda. Hizi ni dalili njema kwa wananchi wetu kwamba watapata fedha za kutosha na kuweza kuboresha hali za Maisha yao kwa kiasi kikubwa. Ninapongeza wananchi waliovumilia hadi kufikia wakati huu ambao bei nzuri imeanza kupatikana. Hapa tunatimiza usemi wa wahenga wa mvumilivu hula mbivu.

**<u>Ombi langu.</u>**

Naomba wananchi wote wa Mtwara kuwapuuza wafanyabiashara wanaoupinga mfumo wa Stakabadhi Ghalani na kuendeleza kununua korosho kwa bei ya chini katika mtindo ujulikanao kama Kangomba au Chomachoma hata wengine kununua korosho zikiwa katika hatua ya maua au zikiwa mbichi.

Naomba wananchi wote tuungane kupigana na biashara hii haramu kwa kauli moja kuwa “Kangomba na Chomachoma ni zilipendewa “Stakabadhi ghalani ndiyo habari ya Mjini” Tukiweka nguvu zetu

pamoja hakika tutafanikiwa kuujenga uchumi na kuongeza kipato chetu.

**Maamuzi ya usafirishaji wa korosho**

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa imefikia makubaliano ya kuzuia usafirishaji wa korosho kwa wakati wa usiku ndani ya Mkoa wa Mtwara. Mwisho wa safari itakuwa saa kumi na mbili jioni. Msafirishji ye yote ndani ya Mkoa anapaswa kusubiri mpaka siku inayofuata.

Naagiza wakuu wa Wilaya zote za Mkoa wa Mtwara, na Kamati za Ulinzi na Usalama kuwa utaratibu huo ufuatwe.

**Ndugu wanahabari.**

Kumekuwepo na uonevu wa baadhi ya vyama vya msingi na maafisa ushirika kuwapunja wakulima malipo yao kwa maelezo au vigezo vya kuwa uzito wa korosho umepungua kutokana na kunyauka. Naagiza kuwa mchezo huo ukome mara moja na mkulima alipwe kulingana na stakabadhi yake aliyopewa pale alipopima korosho zake kwenye chama cha msingi. Kama kutakuwa na upungufu wowote wa uzito basi chama cha msingi ndiyo kibebe mzigo.

**Hali ya Bandari ya Mtwara**.

Leo (3/11/2017) nimetembelea bandari ya Mtwara na kujiridhisha na shughuli za usafirishaji wa korosho unaoendelea. Kusema kweli hali inatia faraja sana. Kwanza upanuzi wa Bandari unaenda vizuri. Serikali imetenga Tsh. 137 Bilioni kwa ajili ya upanuzi wa Bandari na kupitia Bandari serikali imeweza kukusanya Tsh. 124 Bilion na bilioni

24 ushuru wa korosho katika msimu wa 2016/2017. Ajira kwa vijana wetu zimeongezeka na ubora wa korosho Kimataifa umeongezeka.

- Ni maagizo ya Mheshimiwa Rais kuwa Bandari ya Mtwara itumike kusafirisha korosho na ni maamuzi ya Mkoa kuwa Bandari ya Mtwara ndiyo iwe njia pekee ya kusafirisha korosho kwa mikoa ya Mtwara na Ruvuma lakini niwakaribishe wafanyabiashara wengine kuitumia Bandari yetu ya Mtwara.

- Mimi Mkuu wa Mkoa wa Mtwara naagiza kuwa Bandari ya Mtwara ndiyo iwe njia pekee ya kusafirisha korosho. Hakuna mtu ye yote au taasisi itakayoruhusu au kutoa kibali cha kusafirisha korosho nje ya mkoa bila ya idhini yangu. Natambua kuwa wanaweza kuwepo wadau au wasafirishaji wenye mtizamo tofauti nawaomba wawe wavumilivu mpaka pale serikali itakapokuwa imetoa mwongozo kuhusu hili. Aidha Ofisi yangu inaendelea kufanya mawasiliano na Wizara kujua kama kuna Waraka au mwongozo ili serikali ya Mkoa isikinzane na utaratibu wa serikali. Hata hivyo ninalo lengo la kuitisha mkutano wa Wadau wa korosho kujadiliana kuhusu hili. Kwa sasa wafanyabiashara waendelee kutumia Bandari ya Mtwara mpaka tutakapowataarifu vinginevyo.

**Uhaba wa Magunia**

Nimepokea taarifa za uwepo wa uhaba wa magunia kwenye vyama vya msingi na kwamba baadhi ya vyama vimeanza kumwaga korosho chini. Nimetembelea baadhi ya maeneo na kushuhudia korosho zimemwagwa chini. Hali hii ikiendelea itaathiri ubora wa korosho na pengine kushusha bei yake. Tarehe 1/11/2017 nilifanya kikao na wajumbe wa bodi ya korosho na kupata taarifa kuwa Bodi ya korosho ndiyo wenye jukumu la kuagiza na kusambaza magunia. Hata hivyo hawajatimiza jukumu hilo kwa kuwa wakati wanapewa majukumu hayo tayari vyama vikuu vya TANECU na MAMCU vilikuwa vimeagiza magunia.

TANECU walikuwa wameagiza magunia milioni moja na nusu (1.5 milioni) na tayari mzabuni alishakabidhi magunia hayo. Kwa upande wa MAMCU kwa maelezo yao wanasema wanamkataba na DIRMA Holding (Ltd) wa kuwaletea magunia milioni moja (1,000,000) kwa kipindi cha msimu 2017/2018. Niliagiza kuletewa mkataba na baada ya kuupitia nilikutana na yafuatayo:-

(i) Mkataba siyo wa magunia milioni moja ni wa magunia 650,000.

(ii) Mzabuni alipaswa kuwa amekabidhi gunia tarehe 30 Septemba, 2017.

(iii) Mzabuni hajatekeleza na hakuna hatua zilizochukuliwa. Hata idadi kamili ya magunia yaliyoletwa na mzabuni haijulikani.

(iv) Bei au thamani ya Mkataba haijulikani. Kipengele kimoja kinasema mkataba ni thamani ya shilingi milioni mia nane lakini kipengele hicho hicho kinasema ni 4480x650,000 ambayo ni sawa na bilioni mbili na milioni mia tisa.

(v) Baadhi ya wajumbe wa Bodi ya MAMCU wamekana kuutambua mkataba huo na wengine kuwa hawajawahi kuuona.

Kutokana na hali hiyo Ofisi yangu imeamua yafuatayo:-

(a) Kwamba, Bodi ya Korosho isilipe pesa zozote kwa DIRMA Holding Ltd kwa kuwa ameshindwa kuleta magunia kwa wakati na kuna utata wa thamani ya mkataba.

(b) Kuwa, bodi kwa kuwa ndiyo yenye jukumu la kusambaza magunia ihakikishe ndani ya kipindi cha wiki mbili kwa njia watayojua wao, magunia yawe yamepatikana na kusambazwa kwenye vyama vya msingi.

(c) Ofisi yangu itaunda kamati ya uchunguzi ya kuibaini taratibu zilizotumika kuingia mkataba na wote waliohusika na kushauri hatua za kufanya dhidi ya wahusika.

Aidha Mkurugenzi wa Bodi ya korosho na Meneja wa MAMCU walete maelezo ya kwa nini wameidanganya Ofisi yangu kwa kuleta taarifa za uongo kuhusu mikataba ya magunia.

Swali ambalo bado sijapata majibu nataka tume nitakayoiunda inisaidie ni kwa nini tunaagiza magunia kutoka nje wakati tuna viwanda vya kutengeneza magunia hapa nchini. Bodi ya korosho inabidi iachane na utaratibu wa kuagiza magunia kutoka nje na kununua magunia yanayozalishwa ndani na magunia yapatikane mapema kabla ya kuanza msimu.

**Ndugu Wana Habari,**

Nimetembelea baadhi ya maghala ya kuhIfadhia korosho kwenye vyama vya msingi na kujionea hali ya maghala na ubora wake. Maghala mengi siyo imara na hayana thamani ya kutunza dhahabu ya Mtwara. Nitoe wito na kuvitaka vyama vyote vya msingi kutumia pesa inayopatikana kutokana na korosho kuhakikisha wanakarabati au kujenga maghala imara. Nimeagiza niletewe taarifa za ukaguzi wa fedha ya shilingi sitini kwa kila kilo ili nione matumizi yake.

Baada ya kuyasema hayo nimalize kwa kushukuru kwa ushirikiano nilioupata kutoka kwa Bodi ya korosho, baadhi ya wananchi na watendaji wa Serikali na niwahakikishie kuwa pamoja tutaijenga Mtwara.

Gelasius Byakanwa

**MKUU WA MKOA**

**MTWARA.**